

## Kupanga kujifunza katika Miaka 11 na 12

Masomo ya wanafunzi wa juu ni wakati wa kusisimua kwa wanafunzi wa Queensland na hatua muhimu katika kujiandaa kwa maisha yao ya baadaye.

Shule hufanya kazi na wanafunzi wa Mwaka wa 10 na familia zao ili kuwasaidia kupanga malengo yao ya elimu, mafunzo na taaluma na kuweka mpangilio wa njia zao wa kupata Cheti cha Elimu cha Queensland (QCE).

## Cheti cha Elimu cha Queensland (QCE)

QCE ni hitimu ya elimu ya juu ya shule ya Queensland. Inatambulika kimataifa na ni ishara ya mafanikio ya kitaaluma na ya kibinafsi.

QCE huruhusu wanafunzi kubuni njia ambayo inawafaa - iwe malengo yao baada ya Mwaka wa 10 ni:

- kusoma katika chuo kikuu
- kupata kazi yenye ujuzi
- kuhudhuria TAFE au mafunzo mengine.

Wanafunzi wanaweza kuchagua kutoka kwenye aina mbalimbali za masomo na kozi, ikiwa ni pamoja na masomo ya Mamlaka ya Mitaala na Tathmini ya Queensland (QCAA), elimu na mafunzo ya ufundi stadi (VET), uanagenzi na mafunzo ya msingi shuleni au kozi nyingine zinazotambulika.

## Je, QCE inafanya kazi vipi?

Ili kupata QCE, wanafunzi wanahitaji kukamilisha kiasi fulani cha kujifunza katika kiwango kilichowekwa, katika muundo uliowekwa, na kukidhi mahitaji ya kusoma na kuandika na kuhesabu:

**Kiasi kinacho-tambulika**

Alama 20 kutoka kwenye kozi za masomo zilizochangia, ikijumuisha:

- Masomo au kozi zilizoendelezwa na QCAA
- sifa za elimu ya ufundi na mafunzo
- masomo yasiyo ya Queensland
- masomo yanayotambuliwa.

**Kiwango kilicho-pangwa**

Ukamilishaji wa kuridhisha, daraja la C au bora, ukamilishaji wa umahiri au sifa, kufaulu au sawa.

**Muundo wa mpangilio**

Alama 12 kutoka kwenye kozi Muhimu za masomo zilizokamilishwa na alama 8 kutoka kwenye mchanganyiko wowote wa:

- Muhimu
- Maandalizi (kiwango cha juu 4)
- Kozi za Nyongeza (kiwango cha juu 8).

**Kusoma na kuhesabu**

Wanafunzi lazima wakidhi mahitaji ya kusoma na kuandika na kuhesabu kupitia mojawapo ya chaguo zilizopo za kujifunza.

## Masomo na kozi

Masomo na kozi mbalimbali zinaweza kuchangia alama za QCE.

Wanafunzi wengi watasoma masomo/kozi sita katika Miaka ya 11 na 12. Watu wengi huchagua kujumuisha kozi za VET kama sehemu ya njia yao ya QCE na wengine huchagua kupanua masomo yao na masomo ya chuo kikuu au kozi zingine zinazotambulika.

Unyumbufu wa QCE unamaanisha kuwa wanafunzi wanaweza kuchagua njia inayofaa ili kuendana na malengo yao.

Ndani ya hitaji la muundo uliowekwa, kuna aina tatu za kujifunza - Muhimu, Maandalizi na Nyongeza. Kiwango kilichowekwa kinapofikiwa, alama zitaongeka kwenye akaunti ya mwanafunzi ya kujifunzia.

### Masomo ya Jumla ya QCAA — Aina ya msingi ya kujifunza

Masomo ya Jumla huwaandaa wanafunzi kwa masomo ya juu, elimu zaidi na mafunzo na kazi. Huchangia **kuongeza alama nne kwa kila somo** kwa QCE na pia kuchangia kwa Cheo cha Uandikishaji cha Juu cha Australia (ATAR). Mifano ni pamoja na Kiingereza, Hisabati ya Jumla, Historia ya Kale, Biolojia na Upanuzi wa Muziki.

### Masomo Yaliyotumika ya QCAA — Aina ya Muhimu ya kujifunza

Masomo yaliyotumika yanazingatia ujuzi wa vitendo na kuwatayarisha wanafunzi kwa elimu zaidi na mafunzo na kazi. Yanaweza kuchangia **mpaka alama nne kwa kila somo** kwa QCE, na Somo moja Lililotumika pia linaweza kuchangia ATAR ikiunganishwa na Masomo manne ya Jumla. Mifano ni pamoja na Kiingereza Muhimu, Hisabati Muhimu, Mafunzo ya Biashara, Ujuzi wa Teknolojia ya Viwanda na Utalii.

### Kozi Fupi za QCAA — Aina ya Masomo ya Maandalizi au ya Nyongeza, kulingana na kozi

Kozi Fupi zinafaa kwa wanafunzi wanaopenda njia za elimu na mafunzo ya ufundi stadi au elimu ya juu na ajira. Zinaweza kuchangia **alama moja ya QCE**, lakini hazichangii kwenye ATAR. Mifano ni pamoja na Kozi Fupi ya Kusoma na Kuandika, Kozi Fupi ya Kuhesabu na Kozi Fupi ya Lugha za Kiasili (Aboriginal) & za Kivisiwa cha Torres Strait.

### Elimu ya ufundi na mafunzo (VET) — Aina ya masomo ya Muhimu, ya Maandalizi au ya Nyongeza, kulingana na kozi

VET huwatayarisha wanafunzi kwa kazi kupitia kujifunza kwa vitendo na ni sehemu muhimu ya elimu ya juu ya shule kwa wanafunzi wengi. Takriban 60% ya wanafunzi wakubwa wa Queensland wanapata sifa za VET. Katika miaka ya hivi karibuni kozi maarufu zaidi zimekuwa za biashara, teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT), ukarimu, ujenzi, uimara wa mwili, na michezo na burudani.

VET pia inaweza kusababisha elimu na mafunzo zaidi na inaweza kuchangia **mpaka alama nane kwa kila kozi ya** QCE. Kiasi cha alama kitatofautiana, kulingana na aina ya sifa. Sifa moja ya VET katika Cheti cha III au zaidi inaweza pia kuchangia ATAR.

### Kozi zingine — Aina ya masomo ya Muhimu, ya Maandalizi au ya Nyongeza, kulingana na kozi

Kozi zingine huruhusu wanafunzi kusoma eneo fulani la kupendeza, kupitia vyeti na tuzo zinazotambulika, au masomo ya chuo kikuu waliyosoma wakiwa shuleni. Alama za QCE na ustahiki wa ATAR zitatofautiana, kulingana na kozi. Masomo yasiyo ya Queensland kama vile Baccalaureate ya Kimataifa au kozi zilizokamilishwa majimbo mengine pia zimejumuishwa katika kitengo hiki.





## Tathmini

Jinsi wanafunzi wanavyopimwa katika Miaka ya 11 na 12 inategemea na kile wanachosoma.

- **QCAA Masomo ya Jumla**

  Masomo ya Jumla yana tathmini tatu za ndani (yaliwekwa na kusahihishwa na shule) na tathmini moja ya nje (iliyowekwa na kusahihishwa na QCAA). Katika masomo mengi, tathmini ya nje huchangia 25% kwa matokeo ya mwisho ya somo. Katika masomo ya Hisabati na Sayansi, tathmini ya nje huchangia 50%. Wanafunzi katika kila somo watafanya tathmini za nje kwa wakati mmoja katika shule kote Queensland.

- **Masomo Yaliyotumikaaliyotumika ya QCAA**

  Masomo Yaliyotumika yana tathmini nne za ndani (zilizowekwa na kusahihishwa na shule). Katika Kiingereza Muhimu na Hisabati Muhimu, mojawapo ya tathmini ni tathmini ya kawaida ya ndani (iliyowekwa na QCAA na kusahihishwa na shule).

- **Kozi Fupi za QCAA**

  Kozi Fupi zina tathmini mbili ya ndani (yaliyowekwa na kusahihishwa na shule).

- **VET**

  Tathmini ya VET itatofautiana, kulingana na aina ya kozi. Inaweza kujumuisha uchunguzi, jaribio la kuandika, kuuliza maswali, sampuli za kazi au maoni ya watu wengine.

- **Kozi zingine**

  Tathmini katika kozi zingine itatofautiana, kulingana na kozi.

## Mipangilio ya ufikiaji na marekebisho yanayofaa

Mipangilio ya ufikiaji na marekebisho yanayofaa (AARA) ni kwa wanafunzi ambao wanaweza kuwa na ulemavu, udhaifu na/au hali ya kimatibabu au hali ya uzoefu ambayo inaweza kuwa kikwazo kwa utendakazi wao katika tathmini. Ikiwa unafikiri mtoto wako anaweza kuhitaji AARA ili kukamilisha tathmini, tafadhali zungumza na shule yao.

## Kuingia kwenye elimu ya juu

Cheo cha Uandikishaji cha Juu cha Australia (ATAR) hutumika kuchagua waliomaliza shule kwa ajili ya kuingia katika elimu ya juu. ATAR inatumika kitaifa na inaonyesha nafasi ya mwanafunzi ikilinganishwa na wanafunzi wengine wanaostahiki ATAR. ATAR ya Queensland hutegemeana na yafuatayo ya mwanafunzi:

- matokeo matano bora ya Masomo ya Jumla, au
- matokeo bora katika Masomo manne ya Jumla, pamoja na Somo moja Lililotumika, au
- matokeo bora katika Masomo manne ya Jumla, pamoja na sifa moja ya VET katika Cheti cha III au zaidi.

Kituo cha Uandikishaji cha Elimu ya Juu cha Queensland (QTAC) hukokotoa na kutoa ATAR kwa wanafunzi wa Mwaka wa 12. Utapata habari zaidi kwenye tovuti yake: www.qtac.edu.au.

## Cheti cha Queensland cha Mafanikio ya Mtu Binafsi (QCIA)

QCIA hutambua na kuripoti mafanikio ya wanafunzi ambao kujifunza kwao ni sehemu ya programu ya kujifunza ya mtu binafsi. Ili kustahiki, ni lazima wanafunzi wawe na ulemavu au ugumu wa kujifunza ambao hautokani na sababu za kijamii na kiuchumi, kitamaduni au kilugha.

## Matokeo na kuripoti

Matokeo ya mwisho ya somo la mwanafunzi na QCE yanaweza kufikiwa katika Tovuti ya Mwanafunzi kupitia tovuti ya myQCE mnamo Desemba - mwishoni mwa Mwaka wa 12.

## Taarifa zaidi

**myqce.qcaa.qld.edu.au**

Tovuti ya myQCE hutoa habari kuhusu masomo na kozi, tathmini na matokeo, vidokezo vya kusoma na zaidi. Zungumza na shule yako kuhusu masomo na kozi inazotoa.

**qcaa.qld.edu.au**

Maelezo zaidi kuhusu mtaala na tathmini ya sekondari ya juu, ikijumuisha mihtasari ya masomo ya QCAA, inapatikana kwenye tovuti ya QCAA.

240461

Agosti 2024

# Elimu ya sekondari ya juu huko Queensland

## Mwongozo kwa wazazi na walezi



Queensland Government

QCAA Queensland Curriculum & Assessment Authority

*Kwa shule zote za Queensland*